# Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya

*Steven Elisamia Mrikaria*

*Ikisiri*

Makala haya yanachambua usawiri wa mwanamke katika baadhi ya kazi za wasanii wa nyimbo za kizazi kipya nchini Tanzania. Mwanamke anasawiriwa kupitia nyimbo za Kiswahili za muziki wa dansi, taarabu, dini na hata Kizazi Kipya kila wakati. Ili kushuhudia namna mwanamke alivyosawiriwa na wasanii wa nyimbo za Kizazi kipya, tunawarejelea wasanii wachache wa nyimbo hizo ili kushadidia kile kinachozungumzwa kuhusu taswira ya mwanamke katika jamii inayomzunguka. Makala yanaegemea katika nadharia ya ufeministi, hususan ufeministi wa Kiafrika, ambapo matatizo ya udhalilishwaji, ukandamizwaji na udunishwaji wa mwanamke wa Kiafrika yanaangaliwa. Makala yanaanza kwa utangulizi ambapo usuli wa uhusika wa wanawake unaelezwa na kubainishwa. Makala yanaangalia kwa ufupi dhana ya mwanamke katika jamii, na kuelezea nafasi ya mwanamke katika nyimbo za Kiswahili za kizazi kipya. Mwishoni mwa makala haya kuna hitimisho linalotoa majumuisho ya mjadala.

## 1.0 Utangulizi

Masuala ya nafasi ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili yamezungumziwa na waandishi mbalimbali kwa mapana yake. Waandishi kama Mwachofi (1987) na Mazrui (1982) wamechambua taratibu na tamaduni zinazochangia katika kumkandamiza mwanamke. Kwa hakika, wanazuoni hawa wanazungumzia taswira ya mwanamke katika muktadha wa kuwatetea na kuwapigania pale wanaponyang'anywa maslahi yao. Aidha, wataalamu hawa wameonesha uwezo wao wa maandishi katika kuhamasisha usawa kati ya mwanamke na mwanamume katika nyanja mbalimbali za maisha.

Minard (1975) anaitazama nafasi ya wanamke kama dhana ya kisiasa inayojitokeza ili kumnyima mwanamke haki na uwezo wa kushiriki katika kufanya maamuzi. Hapa Mohamed anaiona taswira ya mwanamke kama ina upekee wa aina yake, kwamba amcishia kudai nafasi au hadhi yake fulani katika jamii. Kwa hiyo, suala la taswira ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili ni suala linalobainisha dhahiri utofauti wake na mhusika mwanamume kwa hali mbalimbali. Morris (1993) ameyamulika haya na akahitimisha kuwa tofauti hizi za taswira ya mwanamke na mwanamume ndizo chanzo cha mgawanyo holela wa majukumu kati ya wanawake na wanamume. Baada ya nchi za Afrika Mashariki kujipatia uhuru wake, waandishi wa fasihi ya Kiswahili waliibua, kutumia na kufuata mtindo wa uandishi wa kazi zao. Mtindo huu ulitofautiana na ule uliozoeleka katika kuwaelezea wanawake.

Japokuwa wasanii wanatumia matukio muhimu ya kihistoria katika kuziumba dhamira zao katika ujenzi wa jamii mpya, hatuoni taswira zuri na ya kuridhisha wanayopewa wahusika wanawake (Matteru, 1980). Vilevile, mwanamke katika jamii ya Watanzania anatazamwa kama chombo cha starehe kwa mwanamume (Matteru, 1982). Anasema, msimamo huu haumpi mwanamke heshima kama mzazi bali ni chombo muhimu kwa mwanamume cha kujitosheleza haja zake za kimwili. Pia hatuoni sababu zinazoridhisha kwa wanawake kusawiriwa ndani ya kazi hizo. Waandishi wamediriki hata, bila huruma, kumchora mwanamke kama kiumbe dhaifu, mnyonge na mfungwa (Mohammed, 1981).

Momanyi (2000) akizichambua kazi za Shaaban Robert, ametuonesha kuwa, mwanamke amechorwa katika mtazamo unaomwelezea kuwa ni wa kumstarehesha, kumpamba, kumpendezesha, kumvutia na kumlea mwanamume na familia nzima, na kadhalika. Masuala ya mwanamke kutohusika na kuangaliwa kwa macho ya kipekee kwa kulinganishwa na mwanamume yanaendelea kuchambuliwa na yataendelea hadi hapo usawa utakapoonekana katika jamii. Kujikomboa huko kunatakiwa kuanzie katika nyanja za utamaduni, siasa, uchumi na hata fikra. Hivyo, nyimbo za kizazi kipya baada ya kupambana na changamoto athari taswira ya wanawake, zitasaidia kupata majibu ya maswali yafuatayo:

1. Ni kwa kiasi gani nyimbo za kizazi kipya zinazingatia kikamilifu masuala ya nafasi ya mwanamke?
2. Ni kwa namna gani wahusika wa nyimbo hizo wamejengwa kwa kufuata usawa wa mwanamke na mwanamume?
3. Kuna uwiano gani katika kazi za wanawake na zile za wanaume katika nyimbo za kizazi kipya katika kutekeleza majukumu yao?

## 2.0 Nadharia Inayoongoza Makala

Makala haya yataongozwa na Nadharia ya Ufeministi, ambayo inaangalia uhusiano uliopo kati ya mwanamume na mwanamke. Aidha, itatubidi kuitumia nadharia hii kwa kulisisitiza tawi moja la nadharia hii, tawi la ufeministi wa Kiafrika, ambalo linashughulikia matatizo ya wanawake wa Kiafrika kwa lengo la kuyatatua matatizo hayo.

Kwa mujibu wa Mackinnon (1991), nadharia ya ufeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, hususani katika nchi za Uingereza na Marekani. Kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao na walikuwa ni watu waliokuwa katika daraja la chini. Vilevile, hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kupiga kura au kuchaguliwa

katika uongozi. Shughuli iliyoonekana kuwafaa wanawake ni shughuli za jikoni. Unyanyasaji huu wa wanawake ndio uliopelekea kuibuka kwa nadharia hii ya ufeministi.

Mackinnon anadai kwamba ufeministi ni nadharia ya kwanza kuibuka kutokana na watu ambao walivutiwa nayo. Nadharia huibuliwa na kundi la watu waliovutiwa na mustakabali wake. Anadai kwamba, yaliyosababisha suala la mwanamke kujadiliwa ni kwamba, kwanza, mwanamke amekuwa, kwa muda mrefu, katika kundi la wanaotawaliwa na wanaume. Pili, mwanamke amefanywa kuwa tegemezi katika jamii, sio kwa sababu za kibiolojia, bali ni kutokana na mfumo dume unaozizunguka jamii zetu. Tatu, kutokana na mgawanyo usio sawa wa majukumu, unaoshabikia mwanamke kuwa katika kiwango cha chini cha kazi zisizo na hadhi, kunasababisha jamii kumwona mwanamke kama chombo na si binadamu kama mwanamume.

Wamitila (2002) ameandika kuwa baada ya wanawake kuona kwamba wamewekwa katika daraja la mwisho kwenye ngazi zote za maamuzi, kama yale ya siasa, uchumi na jamii, ndipo walipoamua kuanzisha harakati za kujikomboa. Mwanzoni mapambano hayo yalipigwa vita sana lakini miaka ya 1800 mpaka 1900 madai yao mengi, kama vile haki ya kupiga kura, na kupata nafasi katika ngazi za uchumi na jamii yalianza kukubalika. Nadharia ya ufeministi inatupa fursa ya kuchunguza na kubaini jinsi asasi za jamii zinavyoshirikiana kutatua au kuendeleza tofauti za kijinsia katika kumsawiri mwanamke kwenye kazi za kifasihi.

Makala yatachota data kutoka katika nyimbo za kizazi kipya na kueleza taswira ya mwanamke. Hii ni pamoja na kuchambua namna mwanamke anavyoonekana au anavyochukuliwa ndani ya jamii mpya. Tunaamini kuwa majukumu ya kupika, kulea, starehe, malezi, uongozi, na kadhalika, ni mambo yanayotakiwa kuwepo kwenye jamii, kwa manufaa ya jamii nzima na si kwa baadhi ya wanajamii. Matini za kurejelea zitakazotumika ni nyimbo zilizochaguliwa na zenye kubeba dhamira mbalimbali zinazoonesha taswira ya mwanamke. Vilevile, baadhi ya nyimbo zinazotetea hadhi na udhalilishwaji wa wanawake zitatumika kama changamoto ya mada hii.

## 3.0 Suala la Mwanamke katika Jamii

Tunapoizungumzia jinsia kwa upande mmoja tunaangalia hali ya watu, wanyama, ndege, mimea, wadudu, na kadhalika kuwa wa kiume au wa kike. Kwa upande wa pili wenye uhakika zaidi tunawahusisha wanadamu. Mwanamke ni mwanadamu wa jinsia ya kike. Kwa kawaida anayeitwa hivyo ni yule aliyefikia utu uzima au amebalehe. Kabla ya hapo huwa anaitwa mtoto wa kike au msichana.

Richard na wenzie (2007) wanaeleza kuwa, masuala ya wanawake yalianza kuzungumziwa katika karne ya 19 na kushamiri katika miaka ya 1960 na 1970 ya karne ya 20. Wataalamu hawa wanasema kuwa, wakati huu ndipo wanawake hususan wa Magharibi walipoanza kuzungumzia masuala hayo katika maandishi. Aidha, pamoja na jitihada hizo bado malalamiko dhidi ya dhuluma, unyanyaswaji na uvunjaji wa haki za wanawake kwa takribani nyanja zote za maisha yalizidi kuongezeka. Kwa mujibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP, 2001), katika Bara la Afrika hususan Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanawake wamewekwa katika kundi la wanyonge na walioachwa nyuma kiasi kwamba, bado hawajafaidi hali ya usawa wakilinganishwa na wanaume katika kupata huduma mbalimbali za kijamii. Mbilinyi na wenzie (1991) wameyaeleza haya wakisema kuwa nchini Tanzania wanawake wanaonewa kuanzia nyumbani, barabarani hadi nje ya jamii nzima.

Msanii wa muziki wa Kizazi kipya Banana Zorro katika wimbo *Mama Yangu* anayapinga maneno hayo akisisitiza kuwa mama ndiye nguzo ya maisha na taa ya kumwangazia kiumbe yeyote maishani mwote. Anakiri kuwa mama ndiye anayeongoza, anayeelekeza na kuisimamia jamii tangu mwanzo wa dunia hadi hivi sasa. Anasema:

> (1.a) ...Mama yangu, wewe ni nguzo maishani mwangu, taa imulikayo mbele yangu, daima milele.................

Msingi huo wa Banana Zorro wa kumsifia, kumheshimu na kumthamini mama ni uwakilishi wa taswira ya jinsia ya kike na ndio unaopiganiwa na wasanii mbalimbali wa kizazi kipya.

## 4.0 Dhana ya Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya

Taswira ya mwanamke katika muziki wa kizazi kipya, imekuwa na bado ni gumzo katika mijadala ya jamii mbalimbali za Kiafrika, kupitia tanzu mbalimbali na nyimbo za muziki wa kizazi kipya zikiendeleza. Nyimbo hizi za muziki wa Kizazi kipya zimekuwa zikiichora taswira ya mwanamke kwa kuiangazia mitazamo, maudhui na dhamira mbalimbali kupitia kwa wasanii mbalimbali wa kiume na wa kike. Wapo wasanii ambao ni jasiri katika kusifia nafasi ya mwanamke kama kiumbe jasiri, mvumilivu, shujaa na mwenye kustahimili shughuli ngumu kama vile kuzaa, kutunza, kukuza na kuendeleza jamii. Wapo wasanii waliotumia muda wao mrefu wakithamini, kusifia na kutangaza mambo mazuri yanayowashughulisha wahusika hawa hususan yale yanayowaumiza na kuwadhalilisha juu ya maisha yao ya kila siku na hata kudiriki kupendekeza wasaidiwe.

Kwa kushadidia hoja hii, tunamwona msanii wa kizazi kipya Ben Pol akiusifia uzuri wa mwanamke kitabia katika wimbo *Nikikupata*. Msanii huyu ameyachambua haya akifananisha na mambo aliyokwishakuyafanya maishani mwake, marafiki aliowahi kuwa nao, warembo aliowahi kushirikiana nao, na wote hawa akawaona hawana manufaa kwake kwa kuwa hawawezi kuwa wavumilivu kama mke wake. Anaendelea akisema:

> (2) ......Uzuri sio sura ma, pozi na maumbile kama wengine wanavyodhani, bali nzuri tabia, hekima na ukarimu wako, busara na imani. Na nikikupata milele nitafurahi, nitaimba nakupenda, nakupenda mpaka mwisho wa uhai wangu................

Katika kifungu hiki cha wimbo huu msanii huyu ameonesha umuhimu wa tabia nzuri, hekima na busara kwa mwanamke mwenye mwelekeo wa kuyamudu maisha yake na ya familia yake. Msanii anafafanua kwa kuwekea msisitizo kuwa uhusika wa mwanamke haujadiliwi kwa kuiangalia sura ya mwanamke, urembo wake na wala mwonekano wake wa nje bali hujitokeza na kujidhihirisha katika matendo na mwenendo wa ndani kabisa wa mwanamke, yaani mwonekano wa ndani.

Katika mfumo wa ubabedume, mwanamke alichorwa akiwa na uwezo mkubwa wa kumstarehesha, kumtumikia na kumzalia watoto mwanamume na hata kumwingizia mali na fedha. Haya na mengine mengi yamelengwa na jamii ya ubabedume kumdhalilisha mwanamke yameangaziwa katika nyimbo za wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Aidha, uchambuzi uliofanywa na Wafeministi umeonekana kutambua kwamba taswira ya mwanamke ni matokeo ya kimuundo katika jamii na sio utofauti wa mwanamke na mwanamume tangu zamani (Koda, 2000; Ngaiza, 2002 na Shayo, 2004).

Kwa upande mwingine, wapo wasanii wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya walioiona taswira ya mwanamke katika muktadha wanaousema msimamo mkali, hivyo kumchora mwanamke kama mtu mwenye mwonekano wa kipekee kabisa. Wamediriki kusema katika nyimbo zao hizo kuwa, endapo mwanamke atakataa au atataka kufanya jambo lake fulani la kimapenzi, la kiitikadi, la kimaendeleo, au hata la kimalezi, lazima atafanya kila linalowezekana na lisilowezekana hadi afanikishe azma yake. Wapo wasanii wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya waliosimamia kumwonesha mwanamke kama mtu anayeweza kuamua jambo lolote ambalo analitaka lifanyike na likafanyika bila kipingamizi. Mmoja kati ya wasanii hawa aliyezungumzia hoja hii ni Mwasiti Athamani (maarufu kama Mwasiti) katika wimbo wake *Nalivua Pendo*. Yeye amesikika akisema:

> (3.a)....... Leo nalivua pendo, nililopenda zamani.
> Nabadili wangu mwendo, ili niwe furahani

Katika kipande hiki kifupi cha maneno ya wimbo huu, tunamwona mwanamke akiamua kujitoa katika penzi alilokuwa akilitumikia kwa muda mrefu. Hapa tunaoneshwa taswira ya mwanamke huyu katika mapenzi ya dhati, ilivurugwa na kuchezewa na mwanamume aliyekuwa akimpenda kwa moyo wake wote. Ukiusikiliza wimbo hadi mwisho, utamwona mwanamke akikerwa na manyanyaso ya mwanamume na hivyo kuamua kujitoa kwenye penzi hilo ili aweze kufurahia maisha. Hali inaonekana kuwa vivyo hivyo katika wimbo wa msanii Esterlina Sanga (almaarufu kama Lina) *Bora Nikimbie*. Msanii huyu anamwonesha mwanamke akifanya maamuzi yanayohusu maisha yake bila kumsikiliza mwanamume. Tunamwona msichana Lina baada ya kuolewa, alionekana kuifurahia ndoa, mapenzi, vicheko na starehe. Baada ya miaka kupita mwanamume aliyekuwa akimpenda kwa moyo wake wote alionekana kubadilika kiasi cha kumfanya Lina kufanya uamuzi mzito maishani mwake wa kuachana na mume wake huyo wa ndoa.

Kwa kuzingatia yaliyoibuliwa hapo juu na mengine mengi tunaona kwamba, wasanii wa nyimbo za muziki wa mizazi kipya wameiangalia taswira ya mwanamke katika nyanja zote za maisha, yaani za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Aidha, taswira ya mwanamke katika nyimbo hizo imezungumziwa, imeghanwa na kuchambuliwa na wasanii mbalimbali, wake kwa waume na kwa mapana na marefu yake. Kila msanii ameichambua taswira ya mwanamke kwa namna, mtazamo na mwonekano anaopenda au kuamini.

Kwa kuwa wengi wa wasanii na wachambuzi wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya wameonekana kumsawiri mwanamke katika muktadha wa kumkandamiza, kumwonea na pia kumsakama kwa kila hali. Katika kipengele kifuatacho tutajadili namna wanamuziki hawa wanavyoichambua taswira ya mwanamke katika mtazamo wa kumchopoa kutokana na ubabedume.

## 5.0 Nafasi ya Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya

Muziki wa kizazi kipya ni muziki unaopendwa sana na vijana ambao ndio hasa huonekana kuwa kizazi kipya au kizazi cha leo (Suriano, 2006 na 2007 na Omari, 2009). Nyimbo za muziki wa kizazi kipya, zinabeba na kusambaza ujumbe mbalimbali ukiwa na lengo la kuionya, kuielimisha na kuifundisha jamii maadili mema kupitia wasanii wa kizazi kipya. Matatizo ya ndani na nje ya jamii zetu yamekuwa mengi kiasi kwamba bila ya msaada kama wa wasanii hawa hatuwezi kupata suluhisho. Magonjwa, maovu, manyanyaso, mapenzi, ufisadi, rushwa ya ngono na zembe, na kadhalika, vimekua tishio kwa jamii zetu.

Wasanii wengi wa muziki wa kizazi kipya wameonesha udhaifu wao katika kuyaonesha, kuyatangaza na kuyatetea majukumu yao ndani ya jamii inayotawaliwa na ubabadume. Ni wasanii wachache sana waliolibeba bango la kumtetea mwanamke ndani na nje ya jamii inayomzunguka. Sababu zilizowapelekea wasanii hawa kufanya hivyo ni kama vile mahangaiko katika kutafuta wapenzi, maisha mazuri, kujitangaza na kutafuta pesa.

Ili kuweza kubainisha uhusika wa mwanamke unavyotangazwa kwa jamii na wasanii kupitia waimbaji wa nyimbo za kizazi kipya, inatubidi kuyaangalia maudhui yanayobebwa na nyimbo zao hizo. Aidha, maudhui tuliyovutiwa kuyachambua ni yale yanayobeba dhamira ambazo zimewasukuma wasanii hawa kumchora wanawake kwa mtazamo chanya.

Katika sehemu hii, tutaangalia taswira na mwonekano wa mwanamke kama kiumbe dhaifu na duni, chombo cha starehe na cha biashara, kiumbe kisichostahili elimu kiumbe tegemezi kiumbe kisichopenda mapenzi na mshawishi, kiumbe kisichokuwa na mapenzi na laghai, na kama mzazi, mlezi mwenye mapenzi na huruma.

## 5.1 Mwanamke Kuonekana Kiumbe Dhaifu na Duni

Mwanamke amechorwa kama kiumbe duni na dhaifu, katika jamii (Chesaina, 1981; Ngaiza, 1991; Mbilinyi, 1996 na Kyimba, 2001). Wanasisitiza kwamba, tabia hii ndiyo inayosababisha kukandamizwa kwa wanawake. Aidha, wanadai kwamba, tangu kale mwanamke hakuwa na sauti juu ya mwanamume katika mfumo mzima wa maisha. Ubabedume, mfumo uliokuwa ukiendeleza unyanyaswaji, ukandamizwaji na udhalilishwaji wa mwanamke, uliendeleza ubabe wake huo hadi ilipofikia karne ya 19. Katika karne hiyo, pakaibuka wanaharakati wa mtandao wa jinsia (TGNP) kwa malengo ya kuonesha makucha ya kumtetea na kumkomboa mwanamke kutoka katika jazanda la ubabedume.

Katika kukamilisha harakati za kumkomboa mwanamke, uhuru wa vyombo vya habari, utandawazi, maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, maendeleo ya kidijiti na soko huria vimeonekana kuchukua hatamu za kuwatetea wanawake. Vilevile mabadiliko ya uongozi ndani na nje ya vyama vya siasa, mapambano dhidi ya ubabedume, makongamano ya kumnyanyua mwanamke na kadhalika vimekuwa chachu ya kueneza changamoto za kuleta mabadiliko ya kijinsia na kusukuma mbele mjadala huu katika fasihi simulizi ya Kiswahili.

Mbilinyi na wenzie (1991) wanatanabahisha kwamba, nafasi ya wanawake imekuwa ikibadilika mara kwa mara na ndio sababu ya kubadilika kwa

majukumu na wajibu wao. Kutokana na hayo, nafasi na mwonekano wao umeonekana kuzungumzia katika kazi mbalimbali za kifasihi kwa namna tofauti.

Farsy (1960) amemuonesha mwanamke katika jamii nyingi za Kiswahili kama kiumbe kinyonge, kisichokuwa na nguvu, kilichokosa uwezo mkubwa wa kufanya kazi zenye kutumia nguvu. Kutokana na hoja yao hiyo, mwanamke amekuwa akionekana kama kiumbe dhaifu chenye kufanya kazi duni, na kinachomtegemea mwanamume. Kutokana na hayo, ndio maana wanawake wengi huachwa majumbani kwa minajili ya kufanya kazi za nyumbani zisizotumia nguvu nyingi.

Akipinga hoja hizo hapo juu, Banana Zorro katika wimbo *Mama yangu* anaonesha kwamba, mama hufanya kazi kubwa sana ya kustahili kusifiwa. Kazi azifanyazo mama awapo nyumbani za malezi, kupambana na masumbufu ya watoto, kuwakataza mambo mabaya wanayotenda na kuwaruhusu kutenda mazuri ni mfano tosha wa ugumu wa kazi za nyumbani.

> (1.b) ......Na hukuchoshwa na wangu usumbufu, muda wako mwingi ulitumia kwa ajili yangu ....Nakumbuka mambo uliyoniruhusu na kunikataza, mazuri ulonifanyia, Nashindwa kushukuru.......

Mistari hii michache ya Banana Zorro, inatanabahisha ugumu wa kazi za nyumbani anazofanya mama, ambazo zinachangia katika kujenga utu mwema wa mwanadamu. Mwanamke ameonekana kuonewa hivyo kwa sababu ya kujishusha au ile tabia ya kujidunisha mbele ya wanaume. Vilevile, hutokea wakati ambapo, wanajiona kuwa na hali mbaya za kiuchumi, hali ambayo huwasababisha wanaume kuwaona duni na dhaifu. Kwa kufanya hivyo, mwanamke analazimika kumnyenyekea mwanamume ilimradi apate chakula na kinga. Udhaifu huu unaosababishwa na wanaume kwa malengo yao binafsi ya kutowaruhusu wanawake kufanya shughuli za kujiingizia kipato ndio chachu ya makala haya kutaka kumwambia ukweli mwanamume huyu.

Upo utamaduni unaochangia kwa kiasi kikubwa kumdidimiza mwanamke kuhusiana na nafasi yake katika jamii. Tamaduni hizo ni zile za kumwona mwanamume kiongozi wa familia na mwanamke kuonekana msaidizi tu. Hapa tunamaanisha wapo wanawake wanaodiriki kusema .... *ngoja baba akija utakoma...* Tamaduni kama hizi zimeangaziwa pia na Lughano (1989) na Ndung'o (1999) katika tafiti zao.

Utamaduni wa kumdharau mwanamke kama kiumbe duni akilinganishwa na mwanamume, unaangaliwa pia na wasanii wa kizazi kipya. Msanii kumweka mwanamke katika nafasi ya chini katika uchumi, dini, sheria na hata katika

mirathi kunahitaji kuangaliwa kwa macho ya kipekee. Haya vilevile yameangaliwa na wasanii wa Ottu Jazz Band katika wimbo wa *Mama*. Sehemu ya wimbo huo inayoonesha kutetewa kwa mwanamke katika suala la mahari inasema:

> (4).......Ondoa wasi oh mama haki ya mtu haipotei sikia we mama, Tuhuma si njema kwa msemo wa kale nawasihi wanandoa wote kufuata sheria sio kunyang'anyana mali mnapotengana naahidi mbele yako, nimalizapo masomo na kupata shahada yangu ya sheria, nitawasaidia kina mama wanaoteseka kama wewe........

Kwa bahati mbaya mtunzi wa wimbo huu hafahamu kwamba, hakuna kifungu cha sheria kinachopinga ukandamizwaji wa mwanamke. Zipo sheria chache tu zinazozuia wanawake kumiliki mali, kuvunja ndoa anapomfumania mumewe, kuvunja ndoa hata kama wanaonewa na kadhalika; sheria nyingi zina ubabedume. Kwa mfano, sheria ya mtoto ya 2002 inampa mama jukumu la kumlea mtoto hadi miaka 7 pindi inapotokea wanandoa kutengana. Kwa sababu ya mfumo dume hapo ndipo mwanamume anapommiliki mtoto aliyezaliwa na mwanamke.

Migogoro mingi ya wanandoa inaonekana kutatuliwa kisheria na si kwa nguvu ya ubabedume. Hii ni kwa sababu wanawake wanaonekana kujua wajibu wao hivi sasa. Kwa kupitia nyimbo zipendwazo, yaani nyimbo za kizazi kipya zenye kuwatetea wanawake, itawafanya kuwa hodari wa kutetea haki zao wanazonyang'anywa na wanaume.

## 5.2 Mwanamke Kuonekana Chombo cha Starehe na Biashara

Balisidya (1982) anasema kwamba, ukandamizaji wa wanawake na wanaume unategemea sana uhusiano wao wa kimapenzi. Mwandishi huyu anabainisha dhamira tatu kuu za uhusika wa wanawake katika fasihi: mwanamke mzaaji na mlezi wa watoto, chombo cha kumstarehesha na kumfurahisha mwanamume na mwanamke kama mali. Mawazo haya ya Balisidya yanatusukuma kuuangalia udhalilishwaji wa mwanamke na uhalisia wa maisha yake ya kila siku katika nyimbo zifuatazo:

Katika wimbo wa Zainab Lipangile anayetumia pia jina la kisanii Zay B. *Mama Afrika* tunaona mawazo ya mwanamke si tu kama mama, bali pia kama ua la faraja lililomo Afrika na linalokubalika machoni mwa walimwengu. Tazama anaposema:

> (5.a) .........Mimi mama Afrika Sauti yangu inasikiika, Afrika, Afrika Afrikax 2 Mama Afrika, nafasi nashika, machoni pa watu, nakubalika, natetea wanawake wa Kiafrika, kimawazo kamwe sitafilisika, watoto wa kike wanabakwa kwa ajili ya pipi pipi na ofa,.........

Zay B anaonekana akiwatetea wanawake kwamba, wathaminiwe na kukubalika miongoni mwa wakaaji wa Afrika. Aidha, mwanamuziki huyu anaonekana kuusifia utajiri huu wa wanawake kuwa wasikubali kudhalilishwa na wanaume kwa kutumia msemo kwamba wasidanganyike na ofa za pipi yaani, vizawadi vidogovidogo. Kwa upande mwingine, Zay B anawahamasisha wanawake kujiepusha na wanaume wadanganyifu kwa sababu kazi yao ni kuziharibu sifa adhimu za mwanamke kilimwengu. Hivyo, tofauti na ilivyozoeleka kwa kazi nyingi za kifasihi, mwanamke katika wimbo huu anasawiriwa kama mwelimishaji mzuri na mtu wa utu bora kama alivyo mwanamume. Aidha, katika wimbo huohuo anaonesha kwamba wanawake ndio wazuri (wa sura) kuliko wanaume na kwamba wanakubalika dunia nzima. Angalia mstari huu:

> (5.b) ....Tumeumbika ulimwengu mzima tunakubalika, tunasikitishwa
> na wasichana wa Kiafrika, siku zinavyozidi wanazidi kuharibika,
> sitosita kuwaelimisha, ......

Masuala anayoyasawiri Zay B hapa yanathibitishwa pia na Masuka (1994) ambaye anaelezea kuwa wanawake katika ngano za Kizulu wanatarajia kuolewa na kuzaa watoto. Wanawake wenye sura nzuri walichukuliwa kama ni hatari na kugombaniwa na wanaume, pia wanawake wasiozaa wanaonekana siyo wa kawaida katika jamii ya Kizulu. Zay B anazipinga tabia hizo za ubabedume wa wanaume kuhusiana na mila hizo potofu na anasisitizia wanawake kujiepusha na tohara kwani itawasababishia kukosa hamu ya kufanya mapenzi na mwanamume na kuwa zumbukuku mara amwonapo mwanamume. Hapa msanii huyu anaonekana kuzipinga tabia za wanawake kutumika kama chombo cha starehe na cha biashara na akiunga mkono kampeni ya kitaifa ya kupambana na ukeketwaji wa wanawake.

Zay B katika Mama Afrika anatukumbusha kuwa mwanamke kuonekana kama chombo cha starehe kunapelekea hata wasichana wadogo kufanya mapenzi na wazee, wanawake kufanya starehe na vijana wadogo na hata wasichana wa shule kufanya mapenzi na wavulana wa mitaani. Katika wimbo wake anapinga na kutoa wito kwa wanawake wote kuwa na msimamo:

> *(5.c)............ tunadhalilishwa na kuonekana, chombo cha starehe,*
> *tujaribu kujitunza, watoto wadogo, tusipende kutembea na wazee,*
> *fuateni wosia hiyo tabia, isiendelee, tuzingatie elimu, wazazi tuwape*
> *heshima watoto watia wazimu ............*

Kwa upandc wa mwanamke kuwa na mapenzi ya kweli, na kisha kutumiwa vibaya na mwanamume kama kiburudisho. Mwasiti katika wimbo wake *Nalivua Pendo* anaibuka na dawa yake akisema:

> (3.b) Leo nalivua pendo, nililopenda zamani, Nabadili wangu mwendo, nami niwe furahani. Nimechoshwa na vitendo, visa na purukushani, Kweli mapenzi uvundo, apendwapo hathamini.....

Katika wimbo wake huu tunamwona Mwasiti akianza kwa purukushani za niache, niache kwa kuonesha kuvua penzi lake hilo ili arudi kwenye thamani yake ya kupendwa. Msanii anaonekana kudhalilishwa, kuaibishwa na kufanyiwa mambo ya kihuni akishindanishwa na wanawake wengine. Hapa Mwanamke anaonekana kutokupendwa na kutumika kwa starehe ya chumbani tu. Msanii ameamua kuachana na mwanamume huyo kwa kulivua pendo kwa sababu kupewa mapenzi ya dhati huhitaji vitendo vya wakati wote, yaani kwenye furaha au majonzi. Msanii Linah anaeleza kuhusu mapenzi ya ulaghai, vituko, vipigo na udanganyifu aliyokuwa akifanyiwa na mpenzi aliyemthibitishia kumpenda kwa kumpigia magoti. Sehemu ya wimbo wake huu uitwao *Bora Nikimbie*, inasema:

> (6) Kama mapenzi ni haya, maomba bora nikimbie naona sura ya furaha, Nimechoshwa na vituko na vipigo, Majeraha kila siku mpenzi wako, Hunithamini

Katika wimbo huo, msanii anamlalamikia mpenzi wake kwamba, alimfuata akambembeleza kwa kupiga magoti. Ila baada ya muda mapenzi yale yakawa karaha na manung'uniko kwa mwanamke huyu. Hii inaonesha kwamba ni muhali wanawake na wanaume kuishi katika maisha ya kusaidiana, kuchukuliana mizigo na kupendana kwa dhati.

Yapo maswali ambayo msanii huyu amejiuliza ndani ya wimbo wake huu: ni kwa nini hunithamini? Jibu lake lilidhihirisha kwamba, mwanamume huyu alikuwa na mwanamke mwingine, jambo lililomfanya mwanamke huyu kumlilia majuto ambaye huja baada ya jambo kutendeka. Wapo wanaume wengine ambao wanapoona wawili wapendanao kwa dhati, hujikuta wakiwatafuta kwa ubaya na vurugu za kimwili. Wazandiki hawa hujikuta wakiwahadaa wapendanao hawa bila kujua kwamba wamegharamiana. Ndipo msanii Tunda Man akaamua kuwaimbia kwamba *Starehe Gharama*. Baadhi ya maneno ya wimbo huu yanasema hivi:

> (7) ......... usisikie la kuambiwa jua starehe gharama, kamwe usiwafate wala bata ukiwa na hela ya nyama, usinifate kwenye starehe usije ukanipa lawama, ntakufwata huko kwenye ku'boost .... usiniombe bia kama hujaja na mimi, .....oya oya kaa ukijua starehe gharama, oya oya kaa ukijua starehe gharama aa kaa ukijua kwambaaa ........

Msanii Tunda man ametaka kuidhihirishia jamii kutokubababaikia watu wasiowafahamu kisha wanatafuta na starehe kwa kupitia msimbo wa ngama, bata, na kadhalika. Maneno ya wimbo huu hayausemi uhusika wa jinsia moja tu, bali yanazitahadharisha jinsia zote kufahamu kuwa, maamuzi ya kushiriki katika starehe yoyote ile yanahitaji gharama. Kiango (1992) anasema kuwa, mwanamke huonekana kitegauchumi au chombo cha biashara endapo atakuwa akileta faida kwa mwanamume. Kitendo hiki cha mwanamke kuwa mtafutaji wa fedha kwa njia ya kuuza mwili wake ndicho tunachokiita biashara ya ukahaba. Uhusika huu wa mwanamke kufanya biashara ya ngono umemsikitisha sana msanii Twenty Percent (20%) katika wimbo wake *Yanini Malumbano*:

> (8) .......Yanini Malumbano, ya nini maneno, Najiweka pembeni naogopa msongamano........Umalaya kasi kashika, anagawa kwa kila rika...... Hebu shika talaka yako nenda nendaa, ..Hata kama zamani nilipenda

Hata hivyo, Twenty Percent (20%) hakuonesha kwamba ukahaba anaousema hapa unaendeshwa na mwanamke au mwanamume. Kwa upande mwingine na tukiuangalia kwa undani, uchochezi wa tendo la ngono inayopelekea umalaya si wa mwanamke peke yake, bali ni wote wawili yaani mwanamume na mwanamke.

## 5.3 Mwanamke Kuonekana Kiumbe Kisichostahili Elimu

Historia inaonyesha kwamba wanawake wanabaguliwa katika viwango vyote vya elimu nchini Tanzania. Upo ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha kutokuwepo na usawa katika uwezo wa kupata nafasi ya masomo katika shule zote (Mbilinyi na wenzie, 1991). Buchert (1994) anadai kuwa, mila na desturi za jamii za Waafrika (Tanzania ikiwemo) zinahimiza kuwa kazi za mwanamke katika jamii zinatofautiana na zile za mwanamume kutokana na kiwango cha elimu wanachofikia. Buchert anasema kuwa katika sehemu nyingi, mwanamke anafundishwa kuwa mlezi bora wa familia, ambapo mwanamume anafundishwa kuwa mume mzuri na kiongozi wa familia. Kutokana na sababu hizo, ushiriki wa mwanamke katika elimu ya darasani ulionekana kuwa si halali, na si haki kwake kuipata elimu hiyo.

Suala hili la elimu ya wanawake halijashughulikiwa sana na wasanii wa kizazi kipya. Hata hivyo Vicky Kamata katika wimbo wake wa *Wanawake na Maendeleo*, anawahimiza wanawake kujituma katika kazi ili waweze kujiendeleza na kuiendeleza jamii inayowazunguka.

> (9) ......Ni nani kama mama, jamani nauliza, Walimwengu naomba nidhihirishieni, nafikiria hakuna aliye kama mama, na tena

> hathaminiwi, hapewi haki yake. .......Tangu enzi za mababu, yaeleweka wazi, mama ndiye mlezi hakuna jamii, amka mwanamke............jamani ofisini mwanamke chapakazi, Mlioko bungeni teteeni, haki zetu tuhimize mabinti wapende shule ili wasijenge jazwa kwa kukosa elimu...........

Kamata anawaamsha wanawake katika usingizi wa kujibidisha katika kufanya kazi na kusoma. Anawaasa wanawake wanaopoteza muda wao kwa kusubiri kuletewa kila kitu na wanaume kuwa wako nyuma ya wakati. Kwamba wakati huu ni wa kuzalisha mali kwa pamoja ili kuwarithisha watoto haki zao za msingi ambazo ni elimu na maisha bora. Aidha, msanii anawashauri wanawake kutambua kuwa, elimu inatakiwa iwe mkombozi kwa mwanamke kutokana na mfumo uliopo wa unyanyaswaji na ukandamizwaji kutoka kwa mwanamume. Elimu hiyo inayohimizwa itaisaidia jamii kuondokana na mawazo na mila potofu za kusema kwamba nafasi hizo alizopewa mwanamke ni kwa mapenzi ya Mungu na ndiyo stahiki yake. Aidha, elimu hiyo itawawezesha wanajamii kujenga mawazo na kutoa fursa sawa kwa wote kujadili na kufanya kazi kwa pamoja bila kubaguana.

Dasgupta (2005) anadai kwamba, mtoto wa kike kuendelea na masomo baada ya kujifungua kwa lengo la kuweka usawa kati ya mwanamume na mwanamke katika elimu ni suala la msingi kabisa. Elimu hiyo itawawezesha wanawake kupanga vizuri maisha yao, kuwa na uamuzi wa kupanga na kutekeleza shughuli zao zikiwemo uzazi wa mpango, kushiriki katika shughuli za kisiasa na matumizi bora ya raslimali zilizopo katika jamii. Ndio sababu msanii Nakaaya Sumari (almaarufu Nakaaya) katika wimbo wa *Mr.Politician* anasema:

> (10) ......Miaka ya juzijuzi uliomba kura zetu, Ahadi nazo ulizimimina Elimu bora, Afya bora, barabara nzuri, Ajira nje nje, Leo sioni mabadiliko hali imekuwa ngumu, Eti wajiita Mr. Politician

Kimsingi kwa kupitia maneno ya Nakaaya, elimu wanayoipata wanawake ina mwelekeo wa kuongeza fursa ya wanawake kupata ajira na kushiriki katika siasa na maamuzi. Elimu itawawezesha wanawake kupanga vizuri utekelezaji wa mambo wanayoahidi, kuwa na uamuzi wa kupanga namna ya kutekeleza shughuli haki zao zinazopotea kila mara. Haki wanazonyimwa kama vile: uzazi wa mpango, kushiriki katika siasa na matumizi bora ya raslimali zilizopo katika jamii hupatikana pindi wanapoelimika.

### 5.4 Mwanamke Kuonekano Tegemezi kwa Mwanamume

Wanawake wanawategemea wanaume hasa wanapokuwa katika matatizo makubwa kama vile kufilisika, kuishiwa, kukosa mahitaji yao muhimu, na

kadhalika. Binadamu kwa kiasi kikubwa hutegemeana katika kila hali, pamoja na kupeana ushauri, kutafuta hifadhi na pia kutafuta misaada ya kujiendeleza.

Wanaume katika jamii za Kiafrika wanajiona wenye nafasi za juu na wamiliki wa njia zote kuu za uchumi. Tunaona pia wanaume na wanawake wanamiliki kila kitu. Umiliki huo huwafanya kujiona wenye maamuzi ya mwisho juu ya majaliwa ya wanawake. Hoja hii haina ukweli wala mashiko kwa vile wakati mwingine tunakutana na wanawake wakimiliki wa mali nyingi na hata kummiliki mwanamume. Hata hivyo, mazingira hayo hayajitokezi sana. Mazingira haya yaliyotengenezwa na watu wachache ndani ya jamii kumtegemeza mwanamke yamembadilisha mwanamke kumtegemea mwanamume kutafuta na kugawanya mali zote ndani ya familia. Haya yamemkera kwa kiasi kikubwa msanii Diamond na kuamua kutubainishia katika wimbo *Nitarejea*. Katika wimbo huu, Diamond anaanza kwa kutuonesha kuondoka kwa baba wa familia, ambapo mwanamke anaoneshwa akimlilia baba huyu, bila kufahamu nafasi yake katika jamii itazibwa na nani. Anasema:

> (11.a)....Huwa nakosa raha, pale nikikosa cha kufanya. Roho yangu inauma, sema ntafanya nini. ..... maneno yako yananfanya, nakosa raha na mawazo ...........Unapokwenda kama ukifika salama, utukumbuke na sisi usisahau kama mkeo na wana, umetuacha na dhiki.......

Kupitia maneno ya wimbo huu tunaona kuwa, mwanamke anapoondokewa na mpenzi wake hata kwa kitambo kidogo hukosa raha, faraja na hata mtegemezi. Hapa pia tunamaanisha kuwa, mwanamume naye hukosa hayohayo anayoyategemea kutoka kwa mwanamke. Kwa upande wa pili, tunamwona mwanamke akitumiwa na Diamond kama mshauri wa mwanamume. Karama hii ya ushauri anayosema Diamond amepewa mwanamke na hutumiwa katika muktadha wa kulinda mali, afya na majukumu ya familia ya kila siku. Haya tunayasikia kutoka kwa msanii Diamond akisema:

> (11.b) .....Vile usijali, naomba chunga sana, ogopa na marafiki, wakikulaghai hata kwa mbegu za mtama, waambie sidanganyiki.....

Kwa upande mmoja mwanamke ni mwoga anapowaza kuwa mwanamume anaweza kuzama katika mawimbi na dhoruba danganyifu za dunia. Vilevile, wanawake hupendezwa na maisha mazuri na maendeleo ya familia wanayoitunza. Haya yanaangaziwa na Sajna katika *Nitarejea* na pia katika Iveta. Katika Iveta, Diamond anayamulika maisha ya mjini na yale ya kijijini na kusema:

> (12) ....Ningojee dia, huku mjini nakutafutia mama, nakutafutia dia. .......Mjini sichoki kutafuta, angalau senti kuja kuzileta, ...wangapi huku mjini wanitaka, ila najua wewe ndio unaningoja ....

Kutegemeana kati ya mwanamke na mwanamume kumedhihirishwa pale ambapo mwanamke anashindwa kujiamulia mambo yake bila kushaurina na mume wake aliyekuwa mbali naye. Utegemezi huo huweza kuisha pale mwanamke atapojikomboa kwa kudai haki ya kutokuwa tegemezi kifikra na kiuchumi kutoka kwednye ubabedume. Hapa tunaoneshwa kuwa, utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume ni dhana potofu na dhaifu ambayo tafiti zinatakiwa kuionesha kila wakati kuwa, imepitwa na wakati. Katika maisha hali tunaweza kutoa mfano kwamba, wapo wanawake kama Margareth Thatcher waziri mkuu mstaafu wa Uingereza, Condoleza Rice, na kadhalika, waliowahi kuwa na madaraka kuwazidi wanaume. Makala yanashauri na kuwaambia wapenzi, waandishi na watafiti wa kazi za fasihi kuwa, sasa imetosha kuichafua nafasi ya mwanamke katika kazi zao. Wakati umefika wa kuwaamsha wanajamii ili waandike kile kilicho na ukweli kuhusiana na wanawake na wanaume kutegemeana kwani dunia ya jana imepitwa na wakati.

## 5.5 Mwanamke Kuonekana Asiye na Mapenzi ya Kweli na Mshawishi

Katika jamii nyingi duniani, mwanamke anaonekana kuwa chanzo cha matatizo ya kimapenzi, kiuchochezi na yale ya kiushawishi. Ushahidi wa hoja hii unashadidiwa na Bob Marley anapoimba *"no woman no cry"* kuonesha kwamba mwanamke ndiye chanzo cha matatizo; kwamba asingalikuwepo, matatizo yasingalikuwepo katika suala la mapenzi. Mwanamke anachorwa katika sura mbalimbali: malaya, mshawishi wa wanaume, msaliti na mbabe wa mapenzi. Mwanamke anaoneshwa kila wakati katika taswira hizo pindi tu anapoonekana kutokuwa na mpenzi wa kudumu (kuwa na mume mmoja) au kuonekana akiwa katika makundi mbalimbali miongoni mwa wanaume (baa, disko na shughuli mbalimbali za kijamii) pasipokuwa pamoja na mume wake. Vilevile, mwanamke huchorwa katika sura ya ushawishi pindi inapotokea wakati mwanamume wake anapokuwa hana kipato cha kuifanya familia yake kumudu maisha ya kila siku. Hali kadhalika jamii humwona mwanamke kuwa hana mapenzi ya kweli pindi anapoonekana kutokuyakubali yale yote yanayoendeshwa na ubabedume. Mwonekano wote huu ameuona Senkoro (1982) na akatueleza kuwa, mwanamke anachorwa, anabainishwa na kusawiriwa katika taswira hizi kutokana na kiu walicho nacho wanaume cha kutaka kuwachezea.

Hoja hii ya Senkoro inapingwa na msanii Judith Wambura (almaarufu Lady Jay Dee) akiyaonesha hayo katika wimbo wake wa 'Wanaume Kama Mabinti.' Sehemu ya wimbo huo ni hii ifuatayo:

> (13).....Mnakula, kunywa na kuvaa, siku zinaenda, Vya bure hupenda kupewa wala hamna fikira. Kila upande wanafiki, Siku zinaenda, Vinywa vimejaa ufitini, Wanaume kama mabinti.........Ninaposema wanaume simaanishi wote, Ila wale wenye tabia, kama za mabinti, Utawaona kwenye magari ya 'mademu' zao ..........Tuwatofautisheje na machangudoa .........

Maneno hayo ya Judith Wambura yanapingana na yale ya Senkoro kwa wanaume kuonekana wakihudumiwa na kushughulikiwa na wanawake wenye uwezo na mali. Wanaume wenye tabia kama hizi huitwa wale wenye kuuza sura na kutoa huduma ya mapenzi kwa wanawake wenye pesa, magari na maisha ya anasa. Katika wimbo huu, msanii anajaribu kuyapinga mawazo hayo akiwaambia wanaume kuzalisha mali na kujiepusha na kupenda kupewa misaada, ya bure. Katika jamii zetu tunamoishi, mara nyingine tunakutana na wanaume wenye kufurahia uhusiano wa kimapenzi na wanawake, ilhali mioyoni mwao wakionekana kutokuwa na mapenzi ya dhati kwao. Aidha, utajiri wa wanawake, maisha ya kifahari ya wanawake na hata fedha zao ndivyo huwa kichocheo cha mapenzi. Mawazo ya wanaume hawa huwa yanajikita katika matumizi ya mali, maisha ya kifahari na biashara ya ngono. Wanaume hawa wasiokuwa na mapenzi ya dhati hudiriki hata kutoa rushwa ya ngono kwa wakuu wa dini, serikali na hata asasi za serikali ili waweze kuwasaidia kutatua matatizo yao ya kazi au ndoa.

Wimbo wa Ally Kiba *Mapenzi Yana-run Dunia* usemao:

> (14).......mwenzio mimi ni mtulivu na kuiba mali ya mtu sijafunzwa, Unadhani kama uliyonipa mimi leo inaniuma, fikira zako ziko vibaya kwa kudhani ya kwamba yule demu nilimpenda, Ni kweli nilimpenda lakini ni kama rafiki wa mtima. Haya uliyofanya leo ikifika kesho utajibu nini kiama. Kwa yote mapendo ni kama kioo aliyokupa niliyaona na mimi nakusaliti ....Unatema bigijii, kwa karanga za kuonjeshwa, najua mwanamke akipenda kapenda kweli mimi na run dunia......

Kwa kupitia maneno ya wimbo huo wa Ally Kiba tunaoneshwa jinsi wanawake na hata wanaume wasaliti, washawishi watakavyoadhibiwa siku ya mwisho yaani kiama. Anayafananisha mapenzi ya namna hii kwa msimbo wa pipi ya kutafuna, kwamba baada ya mapenzi yao yasiodumu utamu kumalizika, wanajutia hasara waliyoipata. Hujikuta wakiachana bila thamani yoyote. Pia, kwa upande mwingine, wasiokuwa na mapenzi ya kweli watashindwa kukwepa hukumu ya kiama, hukumu ambayo hivi sasa ni ya hapahapa duniani. Ally Kiba anatuasa kuwa mapenzi ni kioo, hivyo huhitaji kuangaliwa kwa macho ya busara. Awezaye kuvuruga asasi za ndoa, kusambaratisha wapendanao,

kuchochea migogoro ya ndoa na kugombanisha wapendanao huyo ni mzandiki mwenye kuwajibika siku ya mwisho.

**5.6 Mwanamke Kuonekana Kiumbe Laghai Kisichohitaji Msamaha**

Taswira mwanamke kama kiumbe asiyekuwa na mapenzi ya kweli na laghai tunaiona mahali pengi katika jamii zetu. Mahali pengi tunamwona mwanamke akihangaika kila pande za dunia, akimsaka mwanamume wa kumtuliza kiu yake, akichambua na kutafuta bwana mwenye mali na kadhalika. Kadhalika tunamwona mwanamume akisawiriwa ka mmiliki wanawake na kuwabadilisha wanawake kama nguo, akishangilia ndoa zaidi ya moja na kuonesha mapenzi yasiyo ya kweli.

Msanii Twenty Percent (20%) katika *Ningekusamehe* aliouimba baada ya kuachwa kimapenzi na mwanamke ambaye alimpenda na akamwoa na kuishi naye. Baada ya kijana huyu kupata kazi Ughaibuni, aliamua kumwacha mwanamke wake huyu nyumbani kwake na kwenda kusaka maisha. Baada ya kazi hiyo, aliamua kurejea nyumbani na ghafla akamkuta mke wake huyo amechukuliwa na mwanamume mwingine. Alihangaika kumtafuta, kumbembeleza ili warudiane bila mafanikio. Baada ya muda mwanamke huyu aliamua kumrudia na kuomba lakini wakati huo mwanamume huyo tayari alikuwa na mwingine (mwenye mapenzi ya kweli). Ndipo sehemu ya wimbo huo ikaendelea:

> (15).....Naomba ondokaaingie mwenye mapenzi ya kweli asije akakukuta, Ningekuwa nawe ila wewe unapenda sana pesa, ...Ningekusamehe ila tayari nimekwisha mpata mwingine, ......Ni nani aliyetaka kunitoa roho penzi likafika mwisho.........

Hapa mwanamke hana mapenzi ya kweli kama alivyotegemewa na mume wake kutokana na tabia ya kupenda pesa. Katika wimbo huu, hatuambiwi kama mwanamke huyu aliachwa au aliachiwa kitu gani cha kumwezesha kujikimu kimaisha akimsubiri mumewe. Vilevile hatuoneshwi kuwa mwanamume huyu alipokwenda Ulaya alikwenda kufanya kazi gani na kwa nani. Swali linatusibu kwamba, tuna uhakika gani kwamba bwana huyu hakuwa kaolewa Ulaya na taikuni mmoja mwanamke? Huku ni kuiangalia jinsia moja na kuishushia lundo la lawama. Kwa upande mwingine, tunamwona mwanamke akitumia ulaghai kutaka kumghilibu mwanamume kwa maneno matamu ya nisamehe. Haya tunayasikia katika sehemu ya wimbo *Ningekusamehe*, ambapo mwanamke anasema:

> (16)...Mimi ya kale achana nayo, Niko chini ya miguu yako, Basi mpenzi, mbona wanipa kazi, bila wewe siwezi nitajawa na simanzi, .....

> Basi nakwimbia usiweze kunikimbia, unajua sina ujanja wa kuachana nawe, kuniacha njiapanda, nitapata kiwewe, huyo mtimue mi unirudie, usiniache nilie, wewe ni wangu mie, .........

Kwa kuangalia maneno ya huyo mwanamke mlaghai, tunashawishika nasi kumwangalia mtunzi wa wimbo huu kwamba, amefanikiwa sana katika kuuchora ughilibu wa mwanamke. Mwanamke huyu anamlaghai mwanamume amtimue mpenzi wake kwa lengo la kurudiana na yule mwenye mapenzi ya pesa. Aidha, katika wimbo huu, tunaoneshwa pande mbili za mapenzi ya mwanamke, yaani mapenzi ya dhati na mapenzi ya ulaghai. Mwanamke wa pili mwenye mapenzi ya dhati anampenda mume wake kwa dhati, ilhali yule wa kwanza ameonekana akichanganya mapenzi, wanaume na tamaa ya fedha.

## 5.7 Mwanamke Kuonekana Mzazi, Mlezi na Mwenye Huruma

Mwanamke anasawiriwa kama mzazi, mlezi, mtu mwenye upendo na huruma na anaonekana kukubalika katika jamii. Aidha, mwanamke anachorwa kama mtu mwenye mapenzi na kiongozi ambaye daima huiongoza jamii (hususan watoto na vijana) kuuona mwanga bora wa maisha yao. Taswira ya aina hii imeonekana na baadhi ya wasanii wa kizazi kipya kama msaada mkubwa kwao, kwani hata hapo walipofikia (kimaisha); hawana zawadi, tuzo au namna maalumu ya kutoa shukrani kwa mzazi huyu. Kwa kupitia wimbo wa *Mama yangu*, msanii Banana Zoro anatuambia:

> (1.c)...... Mawazo yako mama yanaongoza maisha yangu, Ni tuzo gani unayostahili, wa kuweza kuthamini, shida zangu usumbufu wangu toka kuzaliwa kwangu, na mpaka leo, nasimama mbele yako mama, unastahili sifa kwa mapenzi uloonesha kwangu tangu nazaliwa......... Na hukuchoshwa na wangu usumbufu, muda wako mrefu ulitumia kwa ajili yangu ....Nakumbuka mambo uliyoniruhusu na kunikataza, mazuri ulonifanyia, Nashindwa kushukuru.......

Kwa hakika, katika wimbo huu, msanii ameshindwa kuficha mambo mengi mazuri yanayofanywa na wanawake (mama yake). Msanii anashindwa la kusema anapoiona jamii ikimshusha hadhi, kumdhalilisha na kumhadaa mwanamke huyu ambaye yeye hana hata malipo ya kumlipa. Hivyo, Banana Zoro anaonesha umuhimu wa mama kama mzazi, mlezi na nguzo ya familia. Hii ni kwa sababu aghalabu msingi mkuu wa maendeleo ya mtoto huanza kujengwa na mama. Mama pamoja na kuwekwa katika nafasi ya chini na mfumo dume wa kijamii, hapa anaoneshwa na msanii huyu kama ndiye aliyeko katika nafasi ya juu katika malezi ya jamii. Mama anachambuliwa kama taa yenye kutoa mwangaza wa kumwongoza mwanajamii katika maisha yake yote.

Kwa ujumla, uhusika wa mwanamke kama tulivyoona katika mjadala huu ni changamano na juhudi kubwa bado inahitajika kumkwamua.

Katika kumjadili mwanamke katika nyimbo za kizazi kipya tunaona kuwa masuala ya huruma, upendo na uvumilivu yamejengwa katika sababu za kimaumbile. Mwanamke amejaliwa kuwa na huruma ingawa kuna kipindi huruma hiyo hutoweka. Hilo aghalabu hujidhihirisha pale tu mtoto yeyote yule anapopatwa na madhara kwa sababu ya uchungu aliopewa katika kuzaa. Hii ndio sababu tunasema, uchungu wa mwana aujua mzazi. Pindi itokeapo hali ya kukosa huruma, basi huwa kuna kisababishi ambacho mara nyingi huwa ni mwanamume. Kwa mantiki hiyo, mwanamke kwa asili ya maumbile na kibiolojia ni mtu mwenye huruma, upendo na uvumilivu wa kiasi kikubwa, wakati aghalabu mwanamume akionekana kuyakosa yote haya.

## 6.0 Hitimisho

Tumeona katika makala haya jinsi mwanamke anavyodhalilishwa, anavyokandamizwa na kuonewa katika nyimbo za Kiswahili za kizazi kipya. Nyimbo nyingi zimemchora mwanamke na kumpa taswira za uzinifu (umalaya), kumstarehesha mwanamume na mfanyabiashara (mpenda fedha). Wanawake wameoneshwa kuwa hawana umuhimu sana katika jamii zaidi ya kuwa walezi wa watoto na watumishi wa wanaume. Baadhi ya nyimbo zinawachora wanaume kama wasimamizi wakuu wa majukumu muhimu katika jamii. Wasanii wa nyimbo za kizazi kipya na wale wa muziki wa injili, muziki wa dansi, taarabu, kaswida, na kadhalika wanao wajibu mkubwa wa kuzikwamua jamii zetu kutoka katika mashimo hayo. Vijana na wazee wanapaswa kujikita kimawazo, kivitendo na hata kifikra katika kutunga na kuimba nyimbo zenye kuionya, kuielimisha, kuikosoa, kuisema na kuikumbusha jamii wajibu wake ili isiendelee kuangamia, kupokonywa na kupokwa rasilimali za kijamii walizonazo. Maudhui yanayobebwa na nyimbo hizi yanaweza kumwokoa mwanamke na akajitoa kwenye majanga ya kuonekana kama chombo cha starehe, mlaghai, malaya na mwenye kumilikiwa na kutumiwa na mwanamume kama apendavyo. Ni majigambo, maghani, mizengwe na vituko vya wasanii wetu vinavyolenga katika kuiburudisha, kuikosoa na kuistarehesha jamii, vitakavyotuwezesha kufikisha ujumbe wa kuzielimisha na kuziokoa jamii zetu.

Aidha, ni kupitia wasanii hawa hawa mwanamume anaweza kuelimishwa ili kuweza kuufutilia mbali mfumo dume ambao kwa kiasi kikubwa umeugubika mfumo mzima wa maisha yaliyokuwa yakiendeshwa tangu mababu zetu, na ambao umeendelezwa katika mfumo mzima wa siasa na itikadi za baadhi ya dini zetu. Wanafasihi Mwachofi (1987) na Mazrui (1982), miongoni mwa

wengine, wameonesha kuwatetea wanawake dhidi ya unyanyaswaji, kunyimwa haki zao, kutumiwa kwao kama vyombo vya starehe na vya kuzalishia mali, kumtumikia mwanamume na kulea watoto.

Muhando (1982) anaeleza kuwa juhudi za kumkomboa mwanamke zitapatikana tu pale watakapoungana na kunuia mamoja. Lakini endapo watakengeuka na kutokuwa na umoja, na hata kuchukiana watazidi kunyanyaswa, kudharauliwa na hata kutumikishwa na mfumo dhalimu. Kwa usemi huu wa Muhando inadhihirisha wazi kuwa mwanamke shurti awe wa kwanza kukataa unyanyaswaji huo na kupambana katika kujikwamua na hali hiyo na sio kungojea kukwamuliwa na mwanamume.

**Marejeo**

Balisidya, M. L. (1982). "The Image of the Women in Tanzania Oral Literature." Katika *Kiswahili* Juz. Na. 49/2, Dar es Salaam: TUKI.

Balisidya, M. L. (1987). "Tanzu za Fasihi Simulizi." Katika *Mulika* Dar es Salaam: TUKI.

*Biblia*. (1989). Nairobi: United Bible Societies.

Buchert, L. (1994). *Education in the Development of Tanganyika*. London: James Currey Ltd.

Chesain. C. (1981). "Women in Africa Drama: Representation and Role." PhD Thesis School of English University of Leeds.

Dasgupta, S. D. (2005). *Women's reaslities, Defining Violence against women by immigration, race and class*. Piscataway: NJ. Rughers University Press.

Farsy. (1960). *Kurwa na Doto*. Nairobi: Kenya Litereature Bureau

Khonje, M. (1979). *Some notes on the Rule of Women on Maintainance of Women Oppression by Men*. Dar es Salaam: BRAULUP.

Kiango, S. D. (1982). "Tamthilia za Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa." katika *Mulika* Juz. 49/2, Dar es Salaam: TUKI

Koda, B. (2000). "The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case study of Msindo Village, Same District." Tasnifu ya Uzamivu (PhD), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kyimba, A. A. (2001). "Gender stereotypes in the Folktales and Provebs of Baganda." Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Lughano, R. (1989). "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mackinnon, C. A. (1991). *Toward A Feminist* Theory of the State. London: Havard University Press.

Masuku, N. (1994). "The role of woman in Folklore with special reference to Zulu folktales": Unpublished Honours Article Pretoria University of South Africa.

Materu, B. (1980). "The image of Women in Oral Literature." Dar es Salaam: BRALUP workshop.

Matteru M. O. B. (1982). "The image of the woman oral literature in Tanzania A survey." katika *Jarida la Kiswahili*. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vol. 49/2.

Mazrui. (1982). *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longman.

Mbilinyi, D. (1996). "Women and Gender Relations In school Textbook." In Mbilinyi et al (eds).

Mbilinyi, M. na Wenzie (1991). *Wanawake Tanzania. Uchambuzi wa Harakati zao za Ukombozi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Minard, R. (1975). *Woman folk and fairy tales*. Boston: M.A Houghton Mifflin Company.

Momanyi, C. (2000). "Suala la Uana katika Utafiti wa Fasihi ya Kiswahili. Katika Utafiti wa Kiswahili." *Makala za Kongamano la Chama cha Kiswahili cha Taifa – Kenya 2002*. Nairobi: Moi University Press.

Morris, P. (1993). *Literature and Feminism*. Oxford Black.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Kibaha: EPD.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP). (2001). *Kuelekea kwenye Usawa: Taswira ya Mwanamke Tanzania*. Dar es Salaam: SARDC

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwachofi, A. K. (1987). *Mama Ee*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndung'o, C. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: University Press

Ngaiza, M.K. (2002). Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study, Tasnifu ya Uzamivu (Haijapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Omari, S. (2009). Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature, Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Richard na wenzie. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi:* Sai Industries Ltd

Senkoro, F. E. M.K. (1982). *The Prostitute in African Literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shayo, R. (2004). "Towards Promoting Gender Equality and Equity in Higher Learning Institution: The Case of the University of Dar es Salaam, Tanzania." katika *Tanzania Journal of Development Studies*, Juz. 5 Na. 3, 53-74.

__________ (2007). "Mimi ni Msanii, Kioo cha Jamii, Urban Youth Culture in Tanzania as Seen Through Bongo Fleva and Hip- Hop," *Swahili Forum* 14 (2007): 207-223.

Suriano, M. (2006). "Hip hop and Bongo Flavour Music in Contemporary Tanzania: Youths' Experiences, Agency, Aspirations and Contradictions," Makala yaliyowasilishwa katika Mkutano wa "Youth and the Global South: Religion, Politics and the Making of Youth in Africa, Asia and the Middle East," Dakar, 13–15 Octoba, 2006.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

## YALIYOMO

Muundo wa Majina ya Mahali katika Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Vituo vya Daladala Jijini Dar es Salaam
*A. Buberwa*........................................................................ 1

Kiswahili kama Nyenzo ya Maendeleo Nchini Kenya
*M. Mukuthuria*........................................................................ 15

Challenges of Language Technology of Kiswahili
*A. Hurskainen*........................................................ 29

Tafsiri Sisisi na Athari zake katika Mawasiliano
*O.J. Omari* ........................................................ 49

Kiswahili na Usalama wa Chakula: Vikwazo vya Lugha
*N.J. Ngowa na S. Ryanga*........................................................ 59

Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili
*L. Herman*........................................................................ 73

Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya
*P. M. Y. Ngugi*........................................................................ 84

Dhima ya Kibwagizo katika Ushairi wa Kiswahili
*C. Momanyi na J. N. Maitaria* ........................................................ 95

Falsafa ya Maisha katika Ushairi wa Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert
*A. Mnenuka*........................................................................ 104

Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya
*S. E. Mrikaria*........................................................................ 122

# TAHARIRI

Katika Juzuu hili la 9 kuna makala kumi. Makala tano yanahusu nyanja mbalimbali za kiisimu na makala nyingine tano yanahusu nyanja za kifasihi. Tunapenda kuyadondoa makala hayo japo kwa ufupi. Makala ya Buberwa yanadai kuwa wataalamu mbalimbali wa isimu waliofanya tafiti mbalimbali kuhusu vipengele vya kimofolojia vya nomino za kibantu, walijikita zaidi katika nomino za kawaida ilhali wakiacha nomino mahususi zinazotaja mahali. Makala haya yanazidi kudai kuwa baadhi ya nomino zinazotaja mahali zina maumbo yake maalumu na zinaweza kuchanganuliwa kimofolojia. Kwa undani zaidi ungana na mwandishi kwa kuzama katika makala yake haya. Makala ya kiswahili kama nyenzo ya maendeleo nchini Kenya yameandikwa na Mukuthuria. Makala haya yanaanza kwa kuweka wazi kuwa shughuli yoyote ya mwanadamu inategemea mawasiliano ya lugha kuliko njia nyingine za mawasiliano. Hoja hiyo inathibishwa na kukua kwa kasi ya matumizi ya Kiswahili katika nchi ya Kenya. Kukua huku kumechangia sana kufanikisha maendeleo ya vijijini (mashambani). Mwandishi amehitimisha makala yake kwa kuainisha vikwazo mbalimbali vinavyokikumba Kiswahili katika maeneo hayo ya mashambani.

Makala ya Hurskainen yanayohusu changamoto za teknolojia ya lugha katika Kiswahili yanaleta upya katika tafsiri, hasa tafsiri za Kiswahili. Kuchunguza mbinu mbalimbali za kutafsiri, kunarahisisha kujua ni njia au mbinu ipi inayoweza kuifikisha lugha mahala pazuri katika tafsiri kwa kutumia teknolojia ya lugha. Mwandishi anazidi kufafanua kuwa mbinu zinazofaa katika Kiingereza na lugha nyingine za ulaya si lazima zifae kutumika katika Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika. Ili kupata uhondo zaidi ungana na mwandishi katika makala yake haya. Makala ya Omari yanaangazia athari za tafsiri sisisi katika mawasiliano. Makala hayo yanaeleza changamoto zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa Kiswahili kama lugha yao ya pili hasa katika uandishi. Makala yanadondoa data kutoka insha 100 kuonesha athari ya lugha mama. Tunakualika kuzama katika makala haya ili kujua athari hizo za lugha mama.

Aidha, Ngowa na Ryanga katika makala yao wanabainisha kuwa usalama wa chakula katika jamii yoyote hutegemea jinsi watu hao wanavyowasiliana ili kupata habari, ujuzi na teknolojia katika jamii. Waandishi wanaweka bayana kuwa katika jamii ya Wakenya, hasa wale wa vijijini, nafasi yao ya kujikwamua kupitia kilimo ni ndogo kutokana na ujuzi wa kilimo kutolewa kwa Kiingereza. Msisitizo mkubwa katika mapendekezo yao ni kutumia Kiswahili kama lugha inayoeleweka na wengi.

Halikadhalika, katika Juzuu hili kuna makala mawili yanayohusu fasihi ya watoto. Herman anajadili dhima ya mwingilianomatini kwenye hadithi za watoto katika Kiswahili. Anaonesha matini mbalimbali zinazoingizwa katika hadithi za watoto na kubainisha dhima ya mbinu hizo. Kwa upande mwingine, Ngugi anaangazia namna nzuri ya kuhimiza na kuwaelekeza watoto katika kusoma fasihi inayowahusu. Makala yanatathmini hali ya vitabu vya ziada nchini Kenya kwa kuzingatia upatikanaji na ufaafu wake. Mwisho mwandishi amependekeza namna watoto wa shule za msingi wanavyoweza kuelekezwa na kuhimizwa kusoma ili kukuza utamaduni wa kusoma.

Makala ya Momanyi na Maitaria yanadai kuwa wataalamu mbalimbali wamekuwa wakitoa maelezo duni kuhusiana na uwiano uliopo kati ya kibwagizo cha shairi na maudhui yanayowasilishwa. Makala haya yanaibua dhima kadhaa za kibwagizo katika ushairi wa Kiswahili na mchango wa kibwagizo hicho katika kuainisha mashairi ya Kiswahili. Mnenuka naye katika makala yake anaibua falsafa ya maisha katika ushairi wa Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert. Makala yake yanaonesha jinsi mawazo ya Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert kuhusu falsafa ya maisha yanavyofanana na kutofautiana. Mwisho, mwandishi ameeleza chanzo na misingi ya kufanana na tofauti za wanafalsafa hao. Mwishoni kabisa mwa Juzuu hili, Mrikaria anaonesha jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika nyimbo za kizazi kipya. Kwa ujumla, makala yanaangalia kwa ufupi dhana ya mwanamke katika jamii kwa kuchunguza nafasi yake. Pengine ili kujua ni kwa jinsi gani mwanamke anachorwa katika nyimbo za kizazi kipya, unashauriwa uzame zaidi katika makala haya.

Tunahitimisha tahariri yetu kwa kuwaalika wasomaji na wanazuoni wa Kiswahili kuzidi kuleta makala zaidi ili tuendeleze uhai wa Jarida la *Kioo cha Lugha*. Tunakutakia usomaji mwema.

**Wahariri**

# MAELEZO KWA WAANDISHI WA MAKALA

**KIOO CHA LUGHA** ni jarida la Kimataifa la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili linalochapisha makala ya fasihi na isimu. Jarida huchapisha ***katika Juzuu moja kila mwaka***. Mlengo wa makala ni fasihi na isimu. Makala juu ya kipengele chochote cha fasihi au simu yanakaribishwa. Makala yanaweza kuandikwa katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

**Makala**: Waandishi wanaombwa kuwasilisha nakala mango mbili za kila makala na nakalatepe kwa kutumia anwani ya barua pepe ya www.iks.udsm.tz. Makala yanapaswa kuwa na kichwa cha makala, jina la mwandishi, Chuo au Taasisi anayofanyia kazi, na anuani ya posta pamoja na barua-pepe. Taarifa hizi ziandikwe juu kwenye ukurasa wa kwanza. Makala yawe yamechapwa kwa kutumia programu ya Word, kukiwa na nafasi 1.5 kati ya mstari na mstari, na kukiwa na pambizo pana pande zote. Ikisiri isiyozidi maneno 150 iwe mwanzoni mwa makala chini ya taarifa zilizotajwa hapo juu.

Makala yatatathminiwa na walau wasomaji wawili bila kuonesha mwandishi ni nani. Epuka utambulisho wowote kumhusu mwandishi, ili wanaoyatathmini wasimfahamu mwandishi. Makala yatarejeshwa kwa mwandishi pale tu ambapo gharama za usafirishaji zimelipwa. Waandishi ambao makala yao yatakubaliwa kuchapishwa watapatiwa nakala moja ya Jarida lenye makala yao pamoja na malopoo kumi ya makala.

Mifano katika makala: Mifano yote, iwe ya isimu au fasihi, inapaswa ama kuandikwa kwa **herufi koza** au kwa *italiki*, na haina budi kufuatwa na 'maana' yake kama inahitajika. Kwa wanaisimu, ishara zinazoruhusiwa ni zile za Alfabeti ya Kifonetiki ya Kimataifa. Iwapo kutakuwa na haja ya kuwa na ishara tofauti ziandikwe kwenye ukurasa tofauti.

*Tanibichini* au *Tanibimwisho*: Tanbihi zitumiwe kwa uwekevu; zisiwe nyingi. Kama mwandishi anatumia tanibihi za mwisho wa makala, zichapwe kwenye ukurasa baidi, zikiwa zimeorodheshwa kwa namba.

*Marejeleo*: Utaratibu wa marejeleo uliozoeleka kwa majarida mbalimbali ndio utumike. Kurejelea andiko katika matini kufanyike kwa kuanza na mwandishi, kisha mwaka, na mwisho tarehe, k.m. Mulokozi (1996:34) au (Mulokozi, 1996:35).

Mwishoni mwa makala, marejeleo yaliyotajwa katika andiko yapangwe kiabjadi. Majina ya vitabu na majarida yaandikwe kwa *italiki* na yale ya makala yawekwe kwenye 'alama za kufungua na kufunga semi' kama inavyoonyeshwa hapa:

Mulokozi M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* DSM: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Mekacha, R.D.K.. (1997). 'Disconnecting Education,' katika *Journal la Linguistics and Language in Education*, 3:95-105. DSM: Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Majedwali, Michoro, n.k.: Majedwali, michoro, ramani na picha vipangwe kwa unadhifu kwenye ukurasa. Mahali pa kuweka majedwali, michoro au ramani paonyeshwe kwa uwazi. Majedwali au michoro isiyokaa vizuri kwenye ukurasa mmoja haitachapwa.

Makala ya jarida hili yanapatikana pia Mkondoni kupitia Wavuti ya Taasisi www.iks.udsm.ac.tz na pia katika mkondo wa Majarida ya Kiafrika www.ajol.info.